# HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

*(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)*

:

Mkoa wa Arusha,
Telegram: Arusha
Simu: 2502737
Nukushi: 2503701
B-Pepe: ded@arushadc.go.tz
Tovuti: www.arushadc.go.tz

Ukumbi wa Wilaya,
S.L.P 2330,
**ARUSHA**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SERA YA VIWANDA NA UWEKEZAJI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA ARUSHA**

**A: TAARIFA YA VIWANDA NA UWEKEZAJI**

Ifuatayo ni taarifa ya utekelezaji wa sera ya viwanda na uwekezaji katika Halmashauri ya Arusha. Ikiwa ni sambamba na sera ya taifa juu ya viwanda na uwekezaji kama ilivyoainishwa kwenye Mpango Wa Pili Wa Maendeleo Ya Taifa Wa Miaka Mitano 2016/17-2020/2021.

Katika utekelezajiwa sera hiyo Halmashauri imekwisha kuanza kufanya mambo yafuatayo; -

**1. KUUNDA TIMU YA UWEKEZAJI NA VIWANDA**

Halmashauri imefanikiwa kuunda timu ya uwekezaji na viwanda iliyojumuisha wataalamu wafuatao; - Mweka Hazina, Afisa Mipango, Afisa Vijana, Mratibu wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi, Afisa Biashara, Afisa Maendeleo Jamii, Afisa Moboresho, Afisa Ardhi na Mwanasheria.  Jukumu kuwa la timu ni pamoja na kutafuta na kuyatambua maeneo ya uwekezaji, kufanya mazungumzo na taasisi mbalimbali zikiwemo mashirika na taasisi za fedha, kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo yatakayo ainishwa na timu.

## 2. HALI HALISI YA VIWANDA

Katika Halmashauri yetu ya Arusha hakuna viwanda vikubwa bali kuna viwanda vya Kati **17,** kati ya hivi viwanda **6** vimeanzishwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 na **241** ni viwanda vidogo vidogo. *Tazama Kiambatisho.*

## 3. KUAINISHA MAENEO PENDEKEZWA YA VIWANDA

Halmashauri kupitia timu inayofuatilia maswala ya uwekezaji, imeendelea kufanyia kazi upatikanaji wa maeneo yatakayotumika kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda. Timu hiyo imefanikiwa kubaini maeneo yafuatayo; -

### ENEO LA MALISHO (MBUGA YA ILKUROT) – KATA YA OLKOKOLA

- Ukuwa wa eneo; 50 ekari
- Limepimwa,
- Halihitaji fidia,
- Lina barabara
- Miundombinu ya Umeme ipo karibu,
- Maji yapo,

Hili lina ukubwa wa ekari **123,610** limepimwa na kutengwa kwa ajili ya malisho ya mifugo pamoja na miundombinu yake.

Halmashauri inakusudia kutenga eneo la ekari **50** kati ya **123,610** kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kusindika mazao ya mifugo kama maziwa, nyama, Ngozi na nk.

- **Shamba la Fil – Kata ya Bwawani**

  Halmashauri na ina eneo lenye ukubwa wa **ekari 8** kwa ajili ya uwekezaji wa kiwanda kidogo cha kusindika mazao ya Kilimo. Katika shamba hilo la Hifadhi Builders Ltd wana **ekari 650** ambazo zimepangiwa matumizi mbalimbali zikiwemo **ekari 10** kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo. Aidha, Halmashauri imekwisha andika barua kwa Hifadhi Builders Ltd kuwasisitiza kuanza ujenzi wa viwanda hivyo, ili kwenda na kasi ya sera ya Viwanda.

- **Shamba la Tanzania Plantations Ltd – Kata ya Bwanani**

  Shamba hili lina hati namba NP 304 & NP 305, lilibatilishwa na sasa wamiliki wamefungua kesi Mahakamani. Halmashauri inakusudia kutengae maeneo ya viwanda katika eneo hilo mara kesi hiyo itakapomalizika na Halmashauri, kuruhusiwa kuendelea na shughuli ya upangaji wa matumizi katika eneo hilo.

- **Shamba la Aga Khan**

  Shamba hili limepimwa lina ukubwa wa zaidi ya **ekari 3,000** na linamilikiwa na Aga Khan Foundation. Shamba limeingizwa ndani ya Mpango Kabambe Wa Jiji la Arusha (Master Plan), shamba lipo katika kata tatu (Mateves, Musa na Oltrumet).

  Katika Mpango Kabambe wa Jiji la Arusha, eneo hili limepangiwa matumizi ya Taasisi (Institutions). Aidha, Mpango Kabambe pia umeonyesha maeneo ya Mateves yametengwa kwa ajili ya Viwanda, hivyo Halmashauri inakusudia kufanya mazungumzo na Mmiliki wa shamba hilo kuona uwezekano wa kufanya uwekezaji wa viwanda katika ukanda huo wa Mateves.

- **Shamba la Oldonyosambu**

  Shamba hili lilikuwa limepimwa na lilikuwa na ukubwa wa **ekari 156**. Kwa sasa limebatilishwa umiliki wake kwa manufaa ya umma, wananchi wanachangia gharama za fidia kwa aliyekuwa mmiliki. Halmashauri itawashawishi wananchi wa kijiji cha Lemong'o kutenga eneo angalao ekari 50 kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kusindika karoti, kwa kuwa wananchi wa eneo hilo wanajihusisha zaidi na kilimo cha Karoti.

## 4. WASIFU WA UWEKEZAJI (INVESTMENT PROFILE),

Halmshauri imetengeneza wasifu huo ulioainisha fursa za uwekezaji zilipo ndani ya Halmashauri. Aidha, wasifu huo umesambazwa sehemu mbalimbali na kutangazwa kupitia tovuti ya Halmashauri www.arushadc.go.tz.

**Jedwali Na. 1: Maeneo ya Uwekezaji**

| NA | MAENEO YA UWEKEZAJI | SHUGHULI ZINAZOKUSUDIWA KUFANYIKA | HALI HALISI YA MAENEO YA UWEKEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1 | Kata ya kiutu, kijiji cha Engorika | • Ujenzi wa soko la kisasa<br>• Uwekezaji unaopendekezwa na Halmashauri ni kuingia ubia na taasisi za fedha<br>• Jengo litakuwa na ghorofa 7 ambapo shughuli mbalimbali za kibiashara zitafanyika | Eneo hili lina ukubwa wa ekari 2.3<br>-Eneo limepimwa na linamilikiwa na Halmashauri<br>-Miundombinu (barabara, umeme maji) ni mizuri |
| 2 | Burka Estate Plot No.558 Block A (Ujenzi wa uwanja wa mpira), na plot | • Ujenzi wa maeneo ya burudani (Recreational centre), viwanja vya michezo mbalimbali, Fitness centers “gymnasium” vitajengwa. | -Eneo limepimwa, lina ukubwa wa ekari 3.27 na lina hati, Linamilikiwa na Halmashauri ya Arusha. |
| | No.181 Block A-Burka (Ujenzi wa shopping Mall) | • Plot No.181 Ujenzi wa shopping Mall | -Eneo limepimwa, lina ukubwa 6002m²<br>-Eneo linamilikiwa na Halmashauri<br>-Miundombinu ni mizuri. |
| 3 | Gomba Estate | • Ujenzi wa kituo cha mabasi | -Eneo limepimwa, lina ukubwa wa ekari 4.4 na lina hati<br>-Eneo linamilikiwa na Halmashauri |

| NA | MAENEO YA UWEKEZAJI | SHUGHULI ZINAZOKUSUDIWA KUFANYIKA | HALI HALISI YA MAENEO YA UWEKEZAJI |
|---|---|---|---|
| 4 | Shimo la Mungu kata ya Laroi | • Kuanzisha vivutio mbalimbali vya kitalii kama vile wanyama, Camp Site, ngoma za asili na vibanda vya kutolea huduma mbalimbali kwa watalii.<br>• Eneo linaweza kukodishiwa mwekezaji kwa maelewano baina ya mwekezaji na Halmashauri na kijiji cha Laroi. | -Eneo halijapimwa linakisiwa kuwa na ukubwa wa takribani ekari 1,000.<br>-Eneo linamilikiwa na kijiji cha Laroi. |
| 5 | Mporomoko ya maji Napuku (Napuku water Falls). Kata ya Kiutu kijiji cha Oldadai. | • Uwekezaji unaokusudiwa ni ujenzi wa maeneo ya kupumzikia, vyoo, camping sites, vifaa vya watalii 'Walking infrastructure'<br>• Halmashauri inatafuta mbia. | Eneo halijapimwa |
| 6 | Ngiresi Water Fall, kata ya Bang'ata | • Uwekezaji unaokusudiwa ni ujenzi wa maeneo ya kupumzikia, vyoo,camping sites, vifaa vya vya watalii 'Walking infrastructure'<br>• Halmashauri inatafuta mbia. | Eneo halijapimwa. |

Pamoja na maeneo yaliyoanishwa katika taarifa hii, Halmashauri bado inaendelea na juhudi za kubainisha maeneo zaidi ya uwekezaji wa viwanda, na kuboresha miundombinu yake.

Aidha, Halmashauri imechukua hatua ya kutambuzi wa wananchi wenye maeneo makubwa na wenye nia ya kuwekeza kwenye sekta ya viwanda. Ili Halmashauri ipeleke miundombinu, na kutangaza kwa kuingiza kwenye wasifu wa uwekezaji wa Halmashauri.

Kushoka N.A

**KNY: MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA**